

Mitindo na Lugha ya Uwasilishaji katika Nyimbo za Jando za Jamii ya Watachoni Kutoka Kenya.

Richard Makhakha Iyaya¹; Prof. Nabea Wendo²; Dkt. Gwachi J. Mayaka³

Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya.

Main author email: richard.iyaya@gmail.com

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kutathmini mitindo ya uwasilishaji na lugha inayojitokeza katika nyimbo za jando katika jamii ya watachoni wa kaunti ya bungoma. Nadharia ya baada ya umuundo ya Derrida (1966) ilitumika katika utafiti huu, nadharia hii ilitumika kwa mkamilishano na ya ubabe-dume ya Maclennes (1998). Utafiti huu ulilenga watahiriwa, wazazi, wanaume Watachoni, wanawake Watachoni na viongozi wa shughuli za jando ya Watachoni wanaotumia nyimbo za jando. Sampuli kusudio pamoja na nasibu tabakishi zilitumika. Jumla ya nyimbo 16 za nyimbo (nyiso na maghani) za jando zilitumika na watafitiwa 45 walirejelewa. Deta iliyokusanywa ilirekodiwa kwenye kanda na video, ikaandikwa, ikachanganuliwa na kutafsiriwa kutoka lugha ya Kitachoni hadi lugha ya utafiti-Kiswahili kisha kuwasilishwa. Utafiti huu ulitumia mbinu za uchunzaji nyanjani, mahojiano, mashauriano na wasimamizi pamoja na uainishaji wa habari kutokana na vyombo vya habari. Vifaa kama vile kamera za picha tuli na za kunasa sauti na video na data kuziwasilisha kwa njia ya maelezo, majedwali na picha tuli. Utafiti huu uligundua kuwa mitindo na lugha inayotumika katika uwasilishaji wa nyimbo za jando ndiyo inayoyafanya kukidhi mahitaji ya tohara hii pamoja na kuipa upekee wake. Utafiti huu ulihitimisha kuwa Viongozi wa shughuli za jando wanafaa wapitishiwe katika semina za mara kwa mara kuangazia na kuimarisha utendaji wao katika uteuzi wa matini, mitindo na lugha mwafaka za utoaji mafunzo kupitia nyimbo za jando katika jamii ya Watachoni. Utafiti huu unapendekeza kuandaliwe warsha kwa mahafala wa jando kila baada ya miaka minne ili kuwahamasisha kuhusu kanuni, mitindo na dhima za nyimbo katika shughuli za jando ya jamii ya Watachoni.

Maneno muhimu: Uwasilishaji, Nyimbo Za Jando, Nadharia, Umuundo.

How to cite this article in APA (6th Edition)

Iyaya, R.M, Nabea, W. Mayaka, J. G. (2021). Mitindo na Lugha ya Uwasilishaji katika Nyimbo za Jando za Jamii ya Watachoni Kutoka Kenya. *Editon Cons. J. Kiswahili*, 2(1), 231-253.

<https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v3i1.225>

UTANGULIZI

Nyimbo vile vile zimebainika kuwa na uhusiano wa karibu na sanaa ya ushairi. Kulingana na Matteru (1981, akinukuliwa na Mburu, 2014), nyimbo ni aina ya ushairi unaoimbwa pekee au kwa kuhusishwa na ngoma au kwa kucheza na mwimbaji wake. Pia anadokeza kuwa nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mapigo na muwala. Wimbo unaweza kuimbwa na mtu mmoja pekee au na wapokezi wake wanaoitikia katika mkarara wake. Nyimbo pia zina mfuatano au utaratibu wa sauti, mwendo, picha au ishara. Shaaban (1958) pia anaongeza kudokeza kuwa ushairi ni nyimbo, mashairi na tenzi. Anabainisha kuwa wimbo ni ushairi mdogo na ushairi kama wimbo mkubwa. Nyimbo pia husemekana kuwa sanaa inayowasilishwa kwa toni ya uimbaji ambapo sauti yake huwa tofauti na vipera vingine vya fasihi simulizi ambavyo hughanwa, kutongolewa na kusemwa kikawaida (Methods na wenzake, 2013). Suala la wimbo na ushairi kuwa na tofauti finyu inayodhihirika katika matumizi na uwasilishaji wake. Vipengele hivi hutumia sauti zilizo na toni zenye mahadhi na utaratibu unaosababisha midundo kwenye uwasilishaji ambao hukusudiwa kuimbwa na kuleta maana ya ujumbe kwa jamii (Thonya, 1978).

Wimbo husheheni sifa bainifu zinazoweza kupitisha ujumbe wake unaokusudiwa. Gill na Waters (2009) na Wamitila (2013: 113), wanasema kuwa wimbo huwa na mwasilishaji, ala au vyombo vinavyoandamna na maneno, matini, hadhira na miktadha inayoendana na wimbo huo kwa mfano jando, unyago, harusi na kadhalika. Kwa mujibu wa sifa hizi, inathibitika kuwa kazi ya kisanaa ya nyimbo hutokana na mazingira na kusudio la mambo ambayo yanamfanya Wamitila kuendelea kusema kuwa hisia na mtunzi hatimaye huzaliwa kutokana na mazingira haya ya wimbo husika. Kuhusiana na hili suala la mazingira, M’Ngaruthi (2008:124 na 125) pia anadokeza kuwa nyimbo zilitumika sana katika

kuendeleza katika sherehe na tamasha za kitamaduni mbalimbali na bado zingali zikiendelea hivyo. Anaendelea kuthibitisha maoni ya Wamitila kuwa nyimbo ni zao la shughuli za binadamu pamaoja na hisia zake hivyo huzingatia miktadha mbalimbali ya maisha inavyoingwa mkono na White (1984).

Vilevile, M’Ngaruthi anadokeza kuwa katika jamii nyingi za Kiafrika, sanaa ya nyimbo na ushairi hurejelewa kama sanaa moja ya nyimbo mawazo ambayo pia yalidokezwa na Mnyampala (1970). Tofauti kati ya tanzu hii huwa ni ya kiistilahi tu kwani zote huwasilishwa kwa mdomo, hupangwa katika misitari na vifungu, hutumia lugha ya mkato, kukaririwa au kughanwa na kuimbwa. Sifa hizi husababisha sanaa hizi kuwa na mitindo na lugha ya uwasilishaji kushabiliana kwa kiwango kikubwa na kusababisha kuwa na baadhi ya vipera au mitindo kama vile maghani kuwa katika sanaa zote mbili. Sauti ambayo huwa ni mitetemeko ambazo zinapofikia masikio ya mpokezi, humchochea mpokezi kutafakari juu ya hali na maisha yake. Wimbo hauhusu tu kuandaa matini bali pia sauti katika tanzu zote za kupitisha ujumbe kama vile densi, historia, opera na maaigizo ambayo hudhihirisha matukio ya maisha kwa kumtafakarisha huku ikiwasha mioto ya hisia ndani ya binadamu.

Kulingana na Wamitila (2013:104, akinukuliwa na Mburu, 2014), kazi ya kisanaa ya nyimbo hutokana na mazingira ambayo hujaa tamathali za kimazingira na huweza kufasiriwa kutegemea ujuzi wa hadhira na mazingira husika. Kitendo hiki cha lugha na mitindo wa uwasilishaji hufanya ujumbe katika nyimbo kueleweka katika mazingira pamoja na tabaka bainifu la wanajamii katika hatua mbalimbali za maisha katika jamii husika wanavyodokeza Barasa na Sure (1993), M’Ngaruthi (2008:124). Watachoni wametumia nyimbo simulizi sampuli ya nyiso na maghani kwa muda mrefu katika

tohara zao. Manju hutumia lugha na mitindo teule kuwasilisha ujumbe katika shughuli zao mbalimbali za jando. Kama ilivyo kawaida, fasihi simulizi huwa kioo cha jamii kinachoangaza masuala muhimu ya jamii kwa kutumia nyimbo kiufundi. Dhima ya mchakato huu huwa kuelimisha, kuadilisha, kuendeleza historia ya jamii na masuala mengine yanayojumuishwa katika matumizi ya nyimbo za jando za Watachoni.

Uwasilishaji wa nyimbo za jando katika jamii hii hufanywa na fanani awe mmoja au kikundi cha wataalamu wa masuala ya jando. Utaalamu huu humwezesha msanii kuhakikisha kuwa washiriki wake wameathirika vilivyo kwa mitindo na lugha inayoeleweka katika miktadha ya mazingira na mila zao. Wamitila (2010) anasema kuwa nyimbo huathiri hisia za wapokezi wake. Kwa mfano vijana wanaoshirikishwa hubidi kuelewa ujumbe katika nyimbo za jando ili wapate mwelekeo bora katika maisha baada ya jando kwani nyimbo za jando huandamana na miviga inayotumiwa na fanani kuwapisha wavulana kutoka hatua ya utoto hadi ya utu uzima.

Nyimbo huwasilishwa kwa hadhira kupitia kuimbwa, kukaririwa au kutongolewa kisanana badala ya usemaji wa kawaida. Hutumia lugha ya kishairi na fani ya wizani, lugha yenye mafumbo na inayoimbwa au kughaniwa kwa mitindo na mipigo maalumu ya sauti ya maneno. Nyimbo huathiri moyo wa msikilizaji kwa njia ya kiajabu kiwango cha hurejelewa kama uchawi jambo ambalo linadhibitishwa na baadhi ya wataalam wa fasihi kama vile Mayoka (1986) anaposema kuwa nyimbo huwa na nguvu zinazoathiri wasikilizaji kiasi cha kusababisha walie, wahuzunike, wapate hisia za furaha na hasira kutokana na athari inayoletwa na uzuri wa lugha inayopangwa na kutolewa kwa mapigo mahsus. Lugha inayotumika katika muktadha wa nyimbo huwa ni ya kipekee na hueleweka katika muktadha wa matumizi pekee. Jamii huweza kuzua nyimbo kwa kuteua maneno au usemi kukidhi mahitaji ya

matumizi katika nyanja mbalimbali za maisha. Kwa hivyo, hali ya kuwa lugha inayotumika katika kuwasilisha mafunzo ya kiitikadi katika jamii nyingi huonekana kuwa tata lakini matumizi haya huwa yamekusudiwa sawa na ilivyo katika lugha za uganga, sheria na katika nyanja zinginezo bainifu.

Tatizo letu la utafiti linajikita katika uelewekaji wa mafunzo yanayowasilishwa kupitia nyimbo za jando katika jamii ya Watachoni. Nyimbo hizi huwasilishwa kwa mitindo mbalimbali sawa na lugha maalum kwa madhumuni ya kutimiza malengo muhimu ya jando katika maisha ya watahiriwa. Viongozi wa nyimbo za jando watatumie mitindo na lugha inayowasilishwa mafunzo kwa njia rahisi lakini kuna madai kutoka kwa jamii zingine na baadhi ya walengwa wa nyimbo hizi za jando kuwa hazieleweki. Kuna wataalamu wengi ambao wamefanya utafiti kuhusu nyimbo za jando wakiangazia maudhui, mabadiliko ya nyimbo hizi kutokana na elimu na masuala ibuka mengine. Utafiti huu ulichunguza na kuhakiki uelewa wa mafunzo kwenye nyimbo za jando na umuhimu wake katika jamii ya Watachoni. Kulifikia lengo hili, utafiti huu ulitathmini mitindo, dhima na maudhui katika matumizi ya nyimbo za jando katika jamii hii.

MAPITIO YA MAANDISHI

Lugha na Mitindo ya Nyimbo

“Uwasilishaji wa ujumbe katika nyimbo huwa na ncha mbili: yaani fanani na hadhira hushirikiana katika kupitisha ujumbe kwa kuitikia, kucheza na kushangilia” (King’ei, 1992; uk.98). Ushirikiano kati ya makundi haya hukamilika na kuwa wa maana kupitia usanii yaani mtindo na lugha inayotumika kupitisha huo ujumbe wa nyimbo. Wakati mwingine, lugha ya mtu huonekana kuwa nyenzo mwafaka sana inapotumika kuwasilisha ujumbe kupitia usemi na matendo. Lugha huweza kutumiwa na mtu kiotomatiki katika kusema au kufanya chochote anachotaka. Hata hivyo, wakati mwingine msemaji

huweza kupata kuwa amekosa lugha inayomwezesha kufikia haja ya malengo yake kifahiwa na katika ulimwengu wake hivyo maneno yake hupoteza maana (White, 1984). Kutokana na mawazo haya ya White, kila jamii huweza kuzua nyimbo kwa kuteua maneno, usemi maalum ili kukidhi mahaitaji ya matumizi ya katika nyanja mbalimbali za maisha yao. Katika uwanja wa tohara iwe ya unyago ama jando, kila jamii hutumia nyimbo katika shughuli zake kwa kutumia mitindo na lugha bainifu inayoitambulisha jamii hiyo ili kutoa kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa. M'ngaruthi (2008:133) alilithibitisha jambo hili anaposema kuwa “nyimbo za tohara zinapatikana katika makabila yote ya Kibantu na mengine kama vile ya Kikalenjin, Maasai na Samburu. Tamasha za kila mwaka za Wabukusu zinajulikana sana.

Lugha huwa na nguvu na uwezo wa kuonyesha mahusiano ya kijamii, mifumo ya utawala, mgawanyo wa mali, mila na desturi na mahusiano kati ya wanaume na wanawake kulingana na inavyoitumiwa na mwasilishaji (Masanjila na wenzake, 2009). Mtindo wa lugha ya uwasilishaji kwa ujumla hurejelea tabia ya utungaji inayopambanua mtunzi mmoja na mwingine katika kazi ya kisanaa. Mtindo huu hurejelea namna mbinu mbalimbali hutumia lugha kuwasilisha ujumbe wake (Gikandi, 2003; Miricho na wenzake, 2008). Kulingana na Wamitila (2003) , mtindo kama mbinu au sifa ya uwasilishaji humwezesha mtunzi kupitisha ujumbe wake kwa njia tofauti na mwingine kwani kila mmoja huteua na kutumia tamathali na misamiati ambayo hukidhi mahitaji ya mawasiliano yake katika miktadha . Uelewa huu ulielekeza uainishaji wa mawasiliano ya nyimbo za jando katika kubainisha maana dhima na maudhui yanayotokana na matumizi yake katika jamii ya Watachoni.

Nyiso hutumika kupitisha ujumbe kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kuimbwa, kughaniwa na kutongolewa

katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile za kazi, za siasa, sherehe za harusi, dini, jando na katika kutoa maelekezi mbalimbali katika malezi (Okumba, 2001). Vipera vya nyimbo kama vile mashairi, nyimbo, maghani, tenzi katika fasihi hutumia lugha inayohusu utaratibu wa maisha ya binadamu kwenye jamii husika. Kulingana na Wanjala (2011), miktadha ya kitamaduni na kihistoria huongoza uteuzi wa lugha ya msanii yeyote kwani lugha husheheni mila, itikadi, amali, tabia katika mawasiliano ya jamii husika. Mawazo haya ya Wanjala yanadhihirisha kuwa nyimbo ni aina ya mitindo inayoafiki malengo ya mawasiliano kulingana na vigezo mbalimbali anavyovibainisha mtunzi ili mafunzo yake yaweze kutumia katika jamii mbalimbali. Uelewa huu unaonekana kukubaliana na Madumulla (1989) anayeona kuwa tofauti katika uwasilishwaji wa nyimbo husababisha ukeketo katika uelewekaji wa ujumbe kwa wanaoutumia katika shughuli zao za kila siku kwa kukusudia au bila kukusudia. Kuchunguza mitindo ya nyimbo aina ya nyiso na hasa inavyotumika kuendeleza na kukamilisha malengo ya jando katika jamii hii ya Watachoni ni suala linalochangia kuelewa dhima na maudhui muhimu ya jando na namna yanavyoafikiwa kwa kutathmini uwezo wa mahafala kuyamudu majukumu yao baada ya jando. Uelewa huu hutokana na namna mtindo wa nyimbo huwa umetuyimika katika uwasilishaji husika.

Mitindo ya uwasilishaji na lugha itumikayo hubainisha aina ya shughuli za sherehe na matambiko yanayotokea katika jamii nyingi za ulimwengu hasa za Kiafrika. Kulingana na Mwaniki (1986), nyimbo hutumika kubainisha matukio ya kitamaduni katika jamii kama vile mazishi, utaratibu wa ndoa na tohara. Kwake, nyimbo hutawala utaratibu wa tohara ya Waembu na husheheni maudhui muhimu kwa jamii hiyo yanayotokana na mitindo na ya lugha inayotumika kwenye uwasilishaji wake. Kutokana na ugunduzi huu, tulipata kuelekezwa katika kuchunguza namna mtindo wa nyimbo za jando

hubainisha na kuendeleza matukio muhimu katika jamii ya Watachoni. Ilibainika kuwa kweli nyimbo hizi katika mitindo yake ya nyiso na maghani, hutumika kibainifu katika kila madhabahu ya hatua mbalimbali za jando ili kupitisha ujumbe unaokusudiwa. Hata hivyo, ilibainika kuwa wakati mwingine, mitindo hii ya nyimbo hizi hutumika kama njia ya kujiburudisha na au kutaniana katika jamii. Athari ya nyimbo katika jamii ya Waembu ilibainika kutokea katika jamii ya Watachoni kwa mitindo na malengo yayo hayo.

Msamiati unaotumika katika nyiso na maghani kupitisha ujumbe hutokana na jamii husika ingawa usanii anaotumia mtunzi anapowasilisha na hivyo mlengwa huhitaji usanii anapokea ujumbe huo (Njogu & Chimerah, 1999). Lakini Miricho na wenzake, (2008) wanasema kuwa mitindo ya uwasilishaji ujumbe ndiyo humvutia mlengwa kuliko maana inayotokana na mawasiliano hayo. Uelewa wa waandishi hawa ulituelekeza vilivyo katika kubainisha namna mtindo wa nyimbo za jando kwa jamii ya Watachoni huweza kuiathiri. Ilibainika kuwa kama ilivyo katika mitindo ya mawasiliano katika hotuba, maigizo na mazungumzo inapotumika katika nyimbo, ujumbe hupokelewa kwa njia tofauti kabisa dhidi ya inapokuwa imewasilishwa kikawaida. Hata hivyo, kufurahi na kushangilia kwa wapokezi wake haimaanishi kuwa ujumbe uliokusudiwa umepokelewa na kueleweka kama ilivyokuwa dhahiri katika utafiti huu bali hutegemea na namna nyimbo hizi hutumika.

Kulingana na Barasa na Sure (1993), ugumu katika nyimbo labda hutokana na mtindo wake inavyotumika katika shughuli zake za kijamii. Sifa za nyimbo kutumia lugha yenye maneno machache na sentensi zisizoafiki kanuni za kisarufi katika upangaji wake kuakisi chanzo cha huo ugumu katika uelewaji wa ujumbe katika nyimbo husika. Nyimbo za jando ya Watachoni huwa ya hii sampuli na ndiyo maana husemekana kuwa hazieleweki na

wanaolengwa lakini zaidi wasiolengwa kwayo. Mawazo ya Sure yalituwezesha kuangazia masuala yanayofanya jamii ya Watachoni kusemekana kuwa jamii siri. Watu wanoitwa Watachoni ni watu wa kipekee ambao kwa njia moja au nyingine, walipoteza lugha yao asili ama waliificha ndani ya ngozi, utamaduni na dini yao. Ni watu walio na falsafa iliyofichika na hii imeathiri maendeleo yao (Lihraw, 2010, Uk.21). Kutokana na usemi huu, ni dhahiri kuwa siyo mila ya Watachoni iliyo na ugumu bali ugumu huu hutokana na mitindo ya nyimbo za Watachoni inayotumika kuiwasilisha ujumbe ambao husemekana kujificha kwenye utamaduni wake. Hili lilifanyiwaa uchunguzi ili kubainisha mitindo ya uwasilishaji wa nyimbo za jando dhidi ya dhima na maudhui lilikuwa suala faafu la kutafitia. Kulingana na wasailiwa wetu, imekuwa bayana namna Watachoni walivyowaruhusu wageni waliotoka katika jamii zingine kuishi na kufanya mambo na mila zao bila kuingilia au kulazimishiwa mila na utambulisho wa Watachoni. Jamii kama vile za Tirik, Abakhayo, Abatukuiika kati ya zingine husemekana walitokana na Watachoni lakini hawafanyi mila kama yao kwa sababu hawakuruhusiwa kuiiga walipoishi nao hapo awali.

Kiswahili sanifu kinachotumika katika utunzi wa ushairi hivi leo kimejikita katika maendeleo ya matumizi ya msamiati uliokopwa kutoka lugha zingine. Hili linadhihirika sana katika nyimbo huru nyingi ambazo msamiati wake hueleweka kwa urahisi. Kila jamii nyingi zikiwemo za Kiafrika zinayo misamiati ambayo aghalabu huwa na istilahi zinazotumika katika fasihi simulizi yao ikiwemo nyimbo na maghani, (Kahigi, 1975). Tamathali hizi huzua misamiati inayohitaji kuchanganuliwa katika muktadha wa lugha husika. Jamii ya Watachoni huwa na misamiati sampuli hiyo ambayo zilitambuliwa na kuainishwa katika utafiti huu ili kubainisha ukweli wa madaid haya ya Kahigi. Kutokana na Mayoka (1986), vipengele muhimu vya fasihi kama nyimbo huathiri mioyo

ya watu kiajabu kutokana na uzuri wa mitindo na lugha ya uwasilishaji wake. Kwa misingi ya madai ya Kahigi, utafiti huu ulichunguza matokeo ya matumizi ya nyimbo za jando kwenye jamii hasa inavyowagusa nyoyo zao. Athari hizi ziliangaziwa haswa walivyotekeleza majukumu na kuishi maisha yao baada ya jando.

Mitindo mbalimbali ya mawasiliano hulenga kufaulisha uelewa wa mafunzo au ujumbe unaopitishwa. Kwa mujibu wa Alembi (1999), uelewa wa mafunzo katika nyimbo huwezekana kupitia uwasilishaji wa ujumbe kwa mitindo na lugha inayoeleweka. Usemi huu wa Alembi ulituelekeza kuchunguza namna lugha na mitindo katika mawasiliano ya nyimbo za jando hufaulisha ama kudhoofisha uelewekaji wake kwa walengwa wake katika jamii ya Watachoni. Uelewa wa hali hii ulikuwa muhimu sana kwani mitindio na lugha inayoeleweka huwawezesha wawasilishaji ujumbe kupatana na wasikilizaji au hadhira yao. Uelewa wa hadhira ndio unaoleta uwiyo wa jamii juu ya imani na utamaduni wao. Hata hivyo, Senkoro (1981) anasema kuwa nyimbo zinazoimbwa nyakati za sherehe mbalimbali kama vile nyakati za mavuno, harusi, jando na unyagoni hufurahisha hadhira yake. Kwa mujibu wa Syambo na Mazrui (1992), hadhira hufurahishwa na ujumbe unaotokana na nyimbo za jando kutokana na mitindo na lugha inayotumika kwa ufasaha. Maoni yao yalituwezesha kutathmini namna viwango vya uelewa wa nyimbo za jando unavyoathiri dhima na maudhui yake kwa watahiriwa wa jando na kwa upanuzi jamii ya Watachoni kwa jumla.

Ni dhahiri kuwa nyimbo kama sanaa hutumia lugha kuonyesha na kueleza jambo, wazo au tukio kwa namna inayovutia hisia kutokana na mpangilio maalum wa maneno yanayoteuliwa. Kulingana na baadhi ya wataalamu, akiwemo Madumulla (1989), kauli za mkato, picha na tamathali zinazowasilishwa na wataalamu kwa

hadhira kupitia njia ya kalima, mazungumzo au kama maandishi huwa miundo mbalimbali ya mawasiliano kupitia nyimbo. Kwa mujibu wa ufafanuzi huu, ni dhahiri kuwa Watachoni hufurahia kushiriki katika uimbaji wa nyimbo za jando pamoja na mafunzo yake kutokana na mitindo yao ya uwasilishaji wanayoelewa kama jamii. Kuelewa na kukubali mafunzo yayo hubainika katika mienendo na matendo ya washiriki baada ya mafunzo hayo. Malengo makuu ya jando katika jamii hii huwa kuwaandaa watahiriwa kwa maisha na majukumu muhimu katika jamii yao baada ya jando.

Jilala (2012) katika utafiti wake alichunguza nafasi ya mwanamke katika jamii kwa akizingatia sitiari za ukimwi na mapenzi katika nyimbo za Bongo Fleva. Utafiti wake huo ulibainisha kuwa sitiari zinazomrejelea mwanamke hubeba dhana tano ambazo huunda taswira kumuashiria mwanamke na nafasi yake katika jamii. Dhana hizo zinazombainisha mwanamke huwa uzuri, utamu, thamani, mvutio na utoto. sifa hizi zilionekana kutumika kitaswira kumdhaliisha na kumdunisha mwanamke kwa kumpa hadhi hasi kwenye jamii. Utafiti huu wake ulidhihirisha kuwa nyimbo huweza kuiathiri jamii kutokana na namna lugha na mitindo yake huwa imetumika kuwasilisha ujumbe husika. Uchunguzi na matokeo yake yaliufaa utafiti huu wetu kwani tulidhamiria kubainisha namna matini ya nyimbo za jando yanavyogawanya majukumu kwa jinsia mbalimbali pamoja na kudhihirisha athari zake katika jamii ya Watachoni.

Mitindo ya uwasilishaji katika ushairi huumba maudhui yake ikiambatana na matumizi ya lugha. Kauli hii iliendelezwa na Mulokozi (1982) na Senkoro (1988) waliposema kwamba kinachofanya maudhui kuwa muhimu katika nyimbo za Kiswahili huwa uwasilishaji wake. Utafiti wetu ulichunguza namna mitindo ya uwasilishaji na matumizi ya lugha inavyochangia kuibua

maudhui katika mawasiliano ya nyimbo jandoni kuthibitisha madai ya wataalam hawa. Momanyi (2014) akiangazia masuala ya wanawake katika jamii miaka hamsini baada ya uhuru wa kisiasa, anakadiriya haja ya kutumia mitindo mwafaka ya uwasilishaji ujumbe wa fasihi na lugha faafu ili mawasiliano yakamilike na kueleweka. Utafiti wa wataalamu hawa ulitupa mwelekeo katika kubainisha namna lugha na mitindo ya uwasilishaji umecheza sehemu kubwa katika kugawanya majukumu katika jamii ya Watachoni.

Mapitio haya ya maandishi yaliyorejelewa katika sehemu hii yamedhihirisha kuwa tafiti nyingi hazijachunguza mitindo ya uwasilishaji na matumizi ya lugha katika mawasiliano ya nyimbo za jando kwenye jamii ya Watachoni. Utafiti huu umefanywa ili kuchangia kuliziba pengo hili kwa kuchunguza namna mitindo na lugha inavyoibua dhima na maudhui katika mawasiliano ya nyimbo za jando miongoni mwa wanajamii Watachoni wanaoishi katika Kaunti Bungoma.

MATOKEO

Mitindo ya Uwasilishaji katika Nyimbo za Jando

Mtindo katika kazi ya fasihi huwa namna ambayo msanii hutunga kazi yake na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni au kaida zilizofuatwa ziwe za kimapokeo au za kipekee (Senkoro 2011). Mtindo katika mawasiliano pia hurejelea sifa ya upekee ambayo huitambulisha kazi ya msanii fulani na kuitofautisha na mwingine (Wamitila 2008). Anavyosema Macha (2013), mtindo hujihusisha na njia yenye upekee ambayo humtambulisha na kumtofautisha msanii mmoja na mwingine. Aidha, mtindo huu hurejelea njia au namna ya kuwasilisha ujumbe kimaandishi au kimazungumzo ili mawasiliano husika yaweze kuleta maana iliyokusudiwa (Mohamed, 2011). Mawasiliano huwa suala pana na maana yake hutegemea mazingira jinsi yanavyoingiliana na kuathiriana na aina ya mitazamo ya wanaowasiliana.

Maelezo haya yananaonekana kuwa sawa na ya Wamitila (2006) anaposema kuwa mtindo unaotumiwa katika mawasiliano hutegemea mawazo au njia ya kuyaangalia masuala fulani anayotaka walengwa wake wabainishe umuhimu wake na kukubaliana nayo. Katika utafiti huu, tulijikita katika mitindo mbalimbali ambayo hutumika kuwasilisha ujumbe wa mawazo, maarifa na hisia katika nyimbo za jando kwenye jamii ya Watachoni.

Nyimbo

Jumla ya nyimbo kumi ya mitindo ya nyiso zilitumika katika utafiti huu. Deta iliyotokana na nyimbo hizo ilitumiwa kuainishia mitindo ya nyimbo, dhima pamoja na maudhui yanayotokana na matumizi yake katika jamii ya Watachoni. Nyimbo hizo ziliwekwa katika kategoria mbalimbali kufuatana na dhima na wakati zinapotolewa katika mchakato wa mawasiliano ya jando. Utafiti huu ulibainisha kuwa nyimbo za sifo hutumiwa na jamii ya Watachoni kusifu jamii na mila yake, kupongeza na kuhimiza watahiriwa na jamii kwa ujumla alivyodokeza msailiwa MU 1. Msailiwa huyu alidokeza kuwa nyimbo za jando ziliwasifu watu, mila na wanyama waliorejelewa katika mila yao. Msailiwa wetu pia alibainisha kuwepo nyimbo zinazoimbwa zikilenga kuzichochea ari na ujasiri katika watahiriwa ili waimudu jando. Alibainisha pia kuwa matumizi ya nyimbo katika jando huchanganuliwa katika hatua zake tatu yaani za matayarisho, za kuingia na za kutoka jandoni. Kila wimbo huwa na dhima maalumu inayoendelezwa katika shughuli hizi za jando kama inavyoelelezwa katika jedwali lifuatalo linadhihirisha aina kumi za nyiso kama zinavyowasilishwa. Nyimbo hizi zilibainishwa kwa ufunguo ambao tuliutumia kurejelea hivyo katambulisha nyimbo zinazotumika kuchangia data na kuibua matokeo na mapendekezo ya utafiti huu kwa kodi zifuatazo: MNNJ (Mtindo (M) wa Nyimbo(N) wa Nyiso (N) za Jando(J)) kuanzia 1 hadi 10. Jedwali hili vilevile limetoa maelezo kuhusu kodi za nyiso zilizotumika katika utafiti huu. Nyiso ya kwanza iliyo na kodi MNNJ 1

ndiyo iliyo katika nafasi ya 1 kwenye Kiambatisho cha 1 | nyiso za jando zilizotafitiwa kwenye utafiti huu
nayo ya kumi (MNNJ 10) ndiyo ya 10 kwenye hicho | zimejitokeza kama ilivyo kwenye ufunguo wa jedwali la 1
Kiambatisho. Marejeleo na Ufafanuzi wa data kuhusu | lifuatalo:

Jedwali la 1

Jedwali la Nyiso Zilizotumika

NO	KODI	JINA LA WIMBO KWA KITACHONI	JINA LA WIMBO KATIKA KISWAHILI	WAKATI WA KUWASILSHA NYIMBO	DHIMA YA NYIMBO	MAHALI PA KUUTOLEA WIMBO
1	MNNJ 1	Chapukeya	Tufanyie Pamoja	Wakati wa matayarisho	Kuhimiza umoja wa jamii	Wakati wa kucheleshwa watahiriwa
2	MNNJ. 2	Lukawanga	Lukawanga	Wakati wa matayarisho	Historia ya jamii	Wakati wa kucheleshwa watahiriwa
3	MNNJ. 3	Sieva Khumasewa	Cheza kwa Mizizi ya Mila	Wakati wa matayarisho	Kuendeleza mila za jamii	Wakati wa kucheleshwa watahiriwa
4	MNNJ. 4	Siwali Wareva	Ungeliuliza	Wakati wa matayarisho	Kumtia mtahiriwa ujasiri	Nyumbani kabla ya kuingia jando
5	MNNJ 5	Masewa	Masewa	Wakati wa matayarisho	Kumtia mtahiriwa ujasiri	Wakati wa kucheleshwa watahiriwa
6	MNNJ 6	Yikwe	Mashariki	Wakati wa matayarisho na baada ya kutahiri	Kuendeleza mila/ historia ya jamii	Wakati wa kusalishwa nyama
7	MNNJ 7	Eka kuyeche	Bado ni Mapema	Wakati wa matayarisho	Kumtia mtahiriwa ujasiri	Wakati wa kutoka mtoni siku ya kuenda kutahiri
8	MNNJ 8	Khwaseva Omunyolo	Tumemtahiri Omunyolo	Baada ya kutahiri/kuingia jando	Kusheherekea mila	Uwanjani pindi anapotahiriwa
9	MNNJ 9	Merinde Wandia	Chui Atanila	Wakati wa kutoka jandoni	Kumtia mtahiriwa ujasiri	Anapoanza safari ya kuenda madhabahu ya kutoka jandoni
10	MNNJ10	Sankaya	Sankaya	Wakati wa kutoka jandoni	Kuendeleza mila ya jamii	Madhabahu ya kutolewa jandoni

Kutokana na uainishaji na uchanganuzi wa mtindo huu wa uwasilishaji nyimbo za jando, ilibainika kuwa huu ndio mtindo uliotumika pakubwa katika Utafiti huu. Utafiti huu ulibainisha kuwa mitindo mingine ya uwasilishaji ilitegemea huu mtindo kukamilisha upitishaji ujumbe. Watahiriwa walibainika kufurahia matumizi ya nyimbo za jando kutokana na kuwa zimetumika kwa miaka mingi kupashia jando katika jamii ya Watachoni. Ilikuwa dhahiri kuwa fanani mbalimbali wa nyimbo hizi walifurahia na kuzielewa maana zote kwa mujibu wa mihimili ya nadharia ya baada ya umuundo na ubabe dume. Kwao watahiriwa ilijitokeza kuwa wengi wao hawakuelewa maana kusudifu wa matini katika nyimbo hizo licha ya kuweza kuzifurahia na kutenda namna ilivyotarajiwa. Vipengele vya lugha kama vile misamiati, misemo, tashihisi, taswira, utohozu, jazanda kati ya vingine katika mtindo huu viliwatatiza watahiriwa kung'amua maana kamili iliyokusudiwa. Wengi badala yake waliweza kupata maana ya kiwango nafsi na husishi inavyoelekezwa kwa mihimili ya nadharia ya baada ya umuundo iliyotumika katika utafiti huu.

Mtindo wa Maghani

Utafiti huu ulibainisha kuwa ushairi wa jando wa Watachoni hutumia pakubwa mtindo wa maghani

kuwasilisha ujumbe muhimu kwa watahiriwa na wanajamii wake kwa jumla. Vilevile huwa na hadhira ambayo hushirikiana na fanani kupitisha ujumbe katika nyimbo ili kuendeleza maudhui na dhima bainifu inayolengwa katika mawasiliano hayo. Ildihirika kuwa mawasiliano haya hufanyika kwa ajili ya kuwapa watahiriwa maarifa ya kuishi kikamilifu kulingana na desturi na mila za Watachoni haswa baada ya jando. Mtindo huu ulibainisha kuwa maghani aina ya sifo yalitumika kuwasifu watu, jamii, mila na kufanua masuala muhimu katika utafiti huu kwa misingi ya mawasiliano ya ushairi wa jando. Vilevile maghani haya yalidhihirika kutumika kukashifu mambo yasiyofaa yanayotokea katika jamii ya Watachoni. Nyimbo za maghani zimechanganyuliwa katika hatua mbalimbali za jando mathalani kabla, wakati wa jando na wakati wa kutoka jandoni. Zimerejelewa kwa kutumia kodi kulingana na ufunguo huu wa Jedwali la 2: M – Mtindo; wa N- Nyimbo; za M- Maghani; ya J- wa Jando. Katika jedwali la 2 lifuatalo, inadhihirika kuwa jumla ya maghani 6 yalitumika katika utafiti huu. Maghani haya yamewakilishwa kwa kodi MNMJ 1 hadi MNMJ 6 yanavyojitokeza katika mpangilio kwenye Kiambatisho cha 2 na kudhihirishwa katika Jedwali hili la 2 lifuatalo:

Jedwali la 2

Jedwali la Maghani Yaliyotumika

No	Kodi	Jina la maghani katika Kitachoni	Jina la maghani katika Kiswahili	Hatua ya Mawasiliano ya Jando	Utanzu wa maghani kwa watahiriwa
1	MNMJ.1	Oluvito Iwa Khocha	Maghani ya mjomba wa mtahiriwa	Kabla ya kuingia jando	kivugo na muktadha

2	MNMJ. 2	Oluvito Iwa Omulongi	Maghani ya mwandaaji wa mtahiriwa	Kabla ya kuingia jando	kivugo/kukashifu
3	MNMJ. 3	Oluvito Iwa Okhuramo yinyama	Maghani ya kumweka mtahiriwa nyama	Kabla ya kuingia jando	Kukashifu/ kivugo
4	MNMJ. 4	Oluvito Iwa Omusevi	Maghani ya Ngariba	Baada ya kuingia jandoni	Sifo ya kivugo/muktadha na kukashifu
5	MNMJ. 5	Oluvito Iwa Esitabicha / Emuchela	Maghani ya Esitabicha/ Mtoni	Wakati wa kutoka jandoni	Sifo ya kivugo/kukashifu
6	MNMJ. 6	Wehulo	Maghani ya Sikia	Kabla ya kutoka jandoni	Kukashifu na tondozi

Lugha itumikayo katika maghani haya haya ya MNMJ 1 husheheni nahau zinazowafanya watahiriwa kukosa kuelewa maana yake moja kwa moja.

Katika maghani MNMJ 2, msanii alidhihirika kujisifu na kusifu nasaba ya kina mamake kupitia maghani aliposema ifuatavyo;

*Mimi Cheseve wa Nakhanu, Mtachoni,
Leo hii umekomaa, tunataka kukuandaa uwe mwanamume,
Sasa wewe siye mtoto mdogo tena, nakuvisha nguo ya utu uzima,
Niliumbwa nikatahiri mchana, sikuogopa kamwe*

Nukuu hii huakisi mwandalizi wa mtahiriwa mtoni anapojisifu kutokana na kuimudu jando kwa ujasiri mbele ya jamii yake mchana kutwa wakati wake. Kwenye maghani MNMJ 3, matumizi ya maghani ya sifo kivugo hujitokeza hasa katika mishororo ya 1 na 2. Kulingana na msailiwa BBU 1, maghani haya hulenga kumwezesha mtahiriwa kubaini kuwa jando ilianza zamani sana enzi za babu zake.

Maghani yalibainika kutumika katika MNMJ 4 ngariba anapojigamba kuwa yeye ndiye aliyemtengeneza kuwa mwanamume kwa kumtahiri. Maghani haya MNMJ 1, 2, 3 na 4 yanathibitisha suala hili pamoja na nyiso zilizorejelewa katika utafiti huu. Mtindo huu ulifaulu kuwachochea watahiriwa kuimudu jando pamoja na kuishi baada ya jando kwa ujasiri hivyo kuiendeleza historia na utamaduni wa Watachoni inavyolengwa na mafunzo ya jando kulingana na mihimili wa ujasiri katika nadharia ya ubabe dume. Katika MNMJ 5, maghani ya sifo kivugo yalibainika kutumiwa na msanii kujivunia kuwa Mtachoni na mmoja wa jamii ambayo haijilinganishi kwa mtu au jamii nyingine inapowapitisha watoto wao katika mila yao kwa ajili ya majukumu muhimu ya kijamii baadaye. Mtindo wa maghani umedhihirika kutumika kuyakemea maovu yanayotendeka katika jamii. Kwa mfano, katika MNMJ 6 - sikia, maovu yanayofanywa na wanajamii katika jamii yameainishwa na kukemewa vikali na fanani akishirikiana na jamii kama hadhira.

Mtindo wa Dayalojia

Mitindo hii ya dayalojia ilidhihirika kusheheni katika nyimbo za jando. Kutokana na deta za utafiti huu, ilidhihirika kuwa katika wimbo MNNJ 1, wahusika fanani na wahusika hadhira wanashirikiana kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa; hawa wote wamejitokeza kama waimbaji na watendaji kwa wakati mmoja. Watahiriwa ambao ndio wanaolengwa kwa ujumbe wa uwasilisho huu pia walishiriki kama wahusika wapokezi katika ushairi huu ilivyodokezwa na wasailiwa MJB 1 na MU 7. Kulingana na msailiwa MU 1, mwasilishaji hulazimika kuunganika na walengwa wa ujumbe yaani hadhira kwa ajili ya kuwasiliana na kupatana. Wawasilishaji hushirikiana na hadhira/jamii ili kupitisha ujumbe unaokusudiwa huku wakiufurahia, kuusisitiza inavyostahili kwa mujibu wa mahitaji ya mila na desturi za jamii husika. Dayalojia ili waweza watahiriwa kuweza kufahamu namna jamii ilivyotilia maanani shughuli ya kuwatoa jandoni. Kiitiko kinarudiwarudiwa na hadhira kuweka bayana furaha yao wanaharakisha kuwapeleka watahiriwa kwenye esitabicha kuwatengeneza.

Utafiti huu ulibaini kuwa dayalojia inapotumiwa, jamii nzima huhusishwa wakiwemo pamoja na wale ambao hawakuipitia tohara ya jando mathalani wanawake, watoto na hata watu wa jamii jirani kwa mujibu wa msailiwa MMT 3. Katika wimbo wa MNNJ 1, mbinu hii imebainika kutumika kwani fanani na hadhira wanapokezana maneno katika wimbo huu kama inavyotumika katika nyimbo zingine za utafiti huu ifuatavyo;

Fanani: Ni Wayumbu wa Mawale

Hadhira: Haahaa, Chapukeya

Fanani: Ni Avasyoya Sebulanengo,

Hadhira: Haahaa, Chapukeya

Fanani: Ni Avamakhanga Wekoye

Hadhira: Haahaa, Chapukeya

Fanani: Ni wa Ekhaaka wa Elumbanya,

Hadhira: Haahaa, Chapukeya

Fanani: Ni Wamakhuli wa Kayoka....

Inavyodhihirishwa katika nukuu hii, mbinu ya dayalojia imetumika kwani wahusika hapa wanapokezana hoja yaani kati ya fanani na hadhira. Deta za utafiti zaonyesha kuwa fanani katika wimbo huu anahimiza koo mbalimbali za Watachoni ziunganike na kufanyia shughuli zao za mila pamoja. Anazitaja moja baada ya nyingine huku hadhira ikiitika kana kwamba inakubaliana na fanani kuwa ndiyo, tufanyie pamoja kwa kusema *haahaa, chapukeya*. Hali hii imedhihirika kutokana na mtagusano wa maneno ambao umetokea kati ya fanani na hadhira katika nyimbo zote katika utafiti huu. Mtindo huu katika wimbo huu ulijenga umilisi na umahiri wa koo za Watachoni pamoja na mahali zinapoishi na kubainisha kuwa ufanisi wa mila hutegemea ushirikiano katika jamii husika. Hili jambo lilikuwa muhimu kwani wao huhitaji mshikamano huu kutekeleza majukumu ya utu uzima katika jamii. Hata hivyo, baadhi ya watahiriwa hawakupa maana halisi ya wimbo huu kwa nguzo ya maana iliyokusudiwa kutokana na nadharia ya baada ya umuundo.

Kutokana na matumizi na uchanganuzi wa mtindo huu, imebainika kuwa watahiriwa huweza kupata maelekezo muhimu kuhusu jando kupitia nyimbo za jando. Dayalojia inayotumika katika nyimbo zote katika utafiti huu imefanya mawasiliano haya yakamilike. Fanani huonekana kuzua masuala mbalimbali yanayohusu maombi ya kutoa baraka pamoja na mawaidha kwa watahiriwa huku hadhira ikiyakamilisha kwa kuyatilia mkazo kwa kuitikia. Uwasilishaji maghani kwa mtindo wa dayalojia huwawezesha watahiriwa kubainisha namna jamii inavyoshirikiana ili kuwaombea maisha mazuri katika utu uzima wao huku ikiwapa mafunzo na kukemea ubaya wowote unaoweza kutokea kwao baadaye.

Mtindo wa Maigizo

Maigizo huwa sanaa katika fasihi simulizi ambayo

watendaji huwa wahusika wanaozungumza na kutenda katika sehemu zao mbalimbali kwa zamu. Mtindo huu hutokea kama mchezo wa kuigiza, miviga, ngomezi, ulumbi, sogu, vichekesho na au maonyesho ya sanaa (Musira, 2015). Katika mtindo huu, maneno huambatana na utendaji au uigizaji kuwasilisha ujumbe na kazalisha maudhui katika kazi ya sanaa. Kulingana na msailiwa MU 4, maigizo hudhihirika kutumika katika nyimbo za jando ya Watachoni kuelimisha, kukejeli au kudhihaki mienendo potovu, kuikosa na hata kuburudisha jamii kwa wakati mmoja. Ilibainika kuwa bora mawasilisho ya nyimbo yawe na wahusika kadhaa wanaochukua majukumu au sehemu

mbalimbali na kuwasilisha kwa zamu. Matumizi ya mtindo huu wa maigizo umedhihirika kutumika katika nyimbo za jando kwenye utafiti huu kwa njia mbalimbali inavyodhihirika katika nyiso na maghani ambayo yamerejelewa katika utafiti huu.

Katika wimbo MNNJ 10, mtindo wa maigizo hutumika kubainisha shughuli zinazofanywa na wanajamii wanapowasafirisha watahiriwa kwenda kutengenezwa kwenye madhabahu ya mto wa kuwatoa jandoni kama inavyojitokeza hapa;

Kitachoni

Fanani: Sangaya watiyo hiyohee,

Hadhira: Haahaa, ha! Haahaaha, haaaaaa,

Fanani: Emila hino hiyohee,

Hadhira: Haahaa, ha! Haahaaha, haaaaaa

Fanani: Esambo hino hiyohee,

Hadhira: Haahaa, ha! Haahaaha, haaaaaa

Fanani: Oli omung'ono kuno hiyohee,

Kiswahili

Twenda haraka kwa mila hiyohee,

Haahaa, ha! Haahaaha, haaaaaa,

Hii mila hiyohee,

Haahaa, ha! Haahaaha, haaaaaa,

Kanuni hizi za mila hiyohee

Haahaa, ha! Haahaaha, haaaaaa,

Ati huku kuwaandaa hiyohee,

Uwasilishaji wa wimbo huu huambatana na kucheza kudhihirisha furaha inayotokana na sababu kuwa jamii inawatoa watahiriwa baada ya kutahiri zaidi ya miezi mitatu. Kiitikio huandamana na kurukaruka na kucheza inavyofuatana na maana ya mada ya wimbo huu yaani *tuende haraka kwa mila tukifurahi*. Kulingana na msailiwa MU 1, wimbo huu huwasilishwa katika hatua ya mwisho ya jando ambapo wanajamii wanaowasafirisha, huimba na kucheza huku watahiriwa wakitembea kifahari katika foleni. Kakai (1992) anaunga maelezo haya mkono akidokeza kuwa wanaume wanaokuwa kwenye msafara huigiza na kucheza wakiwa wamevalia mavazi ya kike, kujipamba na kutenda watendavyo wasichana katika jamii yao. Shughuli hii hudhihirisha upekee wa shughuli ya jando inavyofungamana na nyimbo na maghani ya jando na miviga yake katika huu muktadha wa mawasiliano.

Watahiriwa aghalabu huchukulia uwasilishaji huu kama utani bila kuyaona mafunzo yanayowalenga hivyo hubaki kuburudika tu zaidi ya kujifunza. Kwa mujibu wa wasailiwa wetu, watahiriwa hutakikana kubaini kuwa wanaume Watachoni wavaapo mavazi ya wanawake huashiria kuwa watoto wao huuacha utoto unaohusishwa na mama na kuingia katika maisha ya utu uzima. Baada ya jando, mtahiriwa hufaa kuvaa mavazi mapya, kulala katika nyumba mpya na kuishi maisha mapya huku akianza kuyatekeleza majukumu mapya katika familia na jamii yake inavyoelekezwa kwa nguzo za ujasiri na umahiri katika nadharia ya ubabe dume.

Mtindo wa maigizo pia ulidhihirika kwenye maghani MNMJ 5 ambao kulingana na mtafitiwa MKJ 1 hutokea katika madhabahu ya *esitabicha* ambapo alisema kuwa ni

mahali patakatifu kulingana na mila ya Watachoni. Alihusisha madhabahu haya na jukwaa la maigizo kutokana na watahiriwa kuvuliwa nguo, kutumbukizwa kwenye maji kama ishara ya kusajiliwa kuwa wanaume Watachoni kamili. Msailiwa aliongeza kubaini kuwa maigizo yanapotokea, viongozi pamoja na hadhira huimba na kucheza. Pia huwasomea watahiriwa kanuni za mila ya Watachoni na kuwafanyia maombezi ili wafaulu katika maisha wakitekeleza majukumu yao ya baada ya jando. Kulingana na Kakai (1992), shughuli hizi zote zinazofanywa huwa katika juhudi za kumjasirisha mtahiriwa kwa kutumia mtindo wa maigizo kwani huwashirikisha viongozi, hadhira na watahiriwa kwa pamoja. Mtindo huu wa maigizo huwawekea watahiriwa ubayana wa namna jamii inavyowajali kutokana na namna wanavyoomba na kuwabariki wafaulu katika maisha yao ya baadaye kikamilifu inavyojitokeza katika MNMJ 5 ifuatavyo;

Fanani: Sisi huwapitishia watoto wetu katika mila yetu
Watoto wetu tunaowatoa jandoni leo,
Tunawaombea mazuri katika maisha yao,
Wasome tena wasome,

Hadhira: Wasome

Fanani: Wapate mali tena wapate,

Hadhira: Wapate,

Fanani: Wabarikiwe tena wabarikiwe,

Hadhira: Wabarikiwe,

Fanani: Watawale tena watawale,

Hadhira: Watawale,

Fanani: Wapate uzao tena wapate,

Hadhira: Wapate,

Fanani: Mimea izaie na izaie,

Hadhira: Izae,

Haya ni maigizo kwenye jukwaa la estabicha ambapo kuna mapokezani kati ya fanani na hadhira kukiwa na watahiriwa. Maghani haya yanaendelezwa kwa maneno na matendo yanayotilia mkazo baraka zinazotolewa kwa watahiriwa wanaombewa ili wafaulu katika masomo, uongozi, biashara, ukulima na mengineyo kama

yalivyobainishwa hapa. Maghani haya ya jando yalitumia mtindo wa maigizo kuwaandaa watahiriwa kuitetea mila na jamii yao kutokana na fanani na hadhira kwenye maghani MNMJ 5 kuwakemea wale wanaoweza kuinuka kinyume cha mafanikio na usalama wa mahafali wao wa jando baadaye. Pia walibaini majukumu yao kama wanaume Watachoni kutokana na matarajio ya kanuni za jando.

Kwa jumla, mawasiliano yote katika nyimbo za jando huchukuliwa kama maigizo kutokana na majibizano ya maneno na matendo. Nyimbo hizi huwasilishwa kwa mtindo ya nyiso na maghani yanayowashirikisha wahusika wanaowasilisha ujumbe ambao huambatana na desturi na mila za jamii yao. Matokeo ya uchanganuzi wa utafiti huu umedhihirisha kuwa mawasiliano yanayowasilishwa kwa maigizo hueleweka na kuwapa watahiriwa pamoja na jamii mafunzo mengi muhimu. Mtindo wa maigizo hubainika kuchukua nafasi ya mawasiliano tekelezi ya nyimbo za jando katika jamii ya Watachoni. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa uwasilishaji wa nyimbo za jando hufanikiwa kuwasilisha mafunzo kwa watahiriwa kutokana na matumizi ya mtindo huu wa kusema na kutenda yaani kuigiza.

Majigambo

Wimbo MNMJ 6 hubainisha kuwa majigambo hutumika kudhihirisha kuwa mila ya Watachoni ilichimbukia Mashariki ambako wao hutazama wanapotahiri. Kulingana na msailiwa MU 1, nyimbo nyingi za jando zinazoimbwa husifia tohara ya jamii yao pamoja na kujitambulisha kwayo huku wakionyesha namna ilivyo na upekee wake kama inavyojitokeza hapa;

Fanani: Mila yetu ilitoka mashariki hehehee,

Hadhira: Haaho, heehee, hehe, ahaaha,

Fanani: Mashariki juu kwa Chimomoi, hehehee

Hadhira: Haaho, heehee, hehe, ahaahai

Katika msitari wa kwanza wa wimbo huu wa jando

unabainika namna fanani anavyoitambulisha mila yao kuwa ilitoka Mashariki kwa Chimomoi. Watachoni hurejelewa kama *avana va Yikwe* yaani watoto wa Mashariki wanapojigamba kwa ajili ya tohara yao ya jando. Kwa mujibu wa wasailiwa wetu, Watachoni huamini kuwa Mashariki ndiko uhai, jua na hata baraka hutokea hivyo mila inayotumika kuwapa mafunzo muhimu na kuwapa baraka wanapowatengeneza jandoni huweza kufana inapotekelezwa kwa kutazama Mashariki. Majigambo katika wimbo huu yanawawezesha watahiriwa kuimarisha elimu kuhusu Mashariki na umuhimu wake hivyo kuimarisha umahiri wao, kujiamini hivyo kuendeleza utamaduni na historia ya jamii mbele inavyoelekezwa kwa nguzo za maana nafsi, inayokusudiwa na maana kamili ya matini katika nadharia ya baada ya umuundo.

Majigambo yanayofanywa wakati wa sherehe ni aina nyingine ambayo inabainika kutumika katika nyimbo za jando. Majigambo haya huhusiana na mambo au hali halisi inayotokea kwenye jamii kama shughuli muhimu. Siku za jando zinapokaribia, washiriki hujitayarisha kuburudishwa wakati wa majigambo. Anayehusika katika majigambo mara nyingi huwa yule kiongozi wa sherehe ingawa hili hutokea mara chache. Majigambo ya aina hii hubainisha namna jamii husika imekuwa shupavu katika sherehe hiyo ya jando tangu zamani. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, msailiwa MKJ 1, alibainisha kuwa majigambo ya viongozi kabla shughuli muhimu za jando hulenga kuwachochea watahiriwa kujiamini na kushiriki ushupavu wa hali ya juu kama inavyobainika katika nyiso na maghani mbalimbali kwenye nyimbo za jando: MNNJ 1, MNNJ 2 na 3, MNNJ 3, MNNJ 4, MNNJ 5,6 na 7. Inabainika kuwa watahiriwa hupata ujasiri, wakajiamini na kujithamini baada ya kuimbiwa na kughaniwa nyimbo hizi hivyo kuweza kukabili kisu cha ngariba na maisha ya baadaye kwa umahiri na uthabiti.

Kutokana na uchanganuzi huu, ni dhahiri kuwa majigambo ya wasanii binafsi na ya kijamii huchangia pakubwa katika kuwatoa watahiriwa woga wa kukabiliana na tohara za kuingia na kutoka jandoni huku wakiafiki mahitaji ya nguzo mbalimbali za nadharia ya ubabe dume na baada ya umuundo. Mawasiliano haya huwafanya wajiamini na kuithamini tohara hii kutokana na majisifu ya wasanii wanaoimudu jando hivyo kuheshimika kwenye jamii wakati wote. Hata hivyo, watahiriwa wameonekana kupata changamoto kubainisha maana ya baadhi ya vipengele vya lugha vinavyofanya uelewa wao kuwa mgumu kutokana na umri mdogo unaowakosesha tajriba kwenye misamiati na matukio yanorejelewa. Kwa mfano, miktadha ya kufanya mapenzi na wake wa wenyewe, kanuni za kumkataza mtahiriwa kushinda nyumbani na mamake, mtahiriwa kupewa mamlaka ya kuilinda familia na jamii, mawe matatu yanayopanda kijiti, wanaogopa jando kwenda Ujaluoni na majina ya sehemu na viongozi mbalimbali katika mila za Watachoni iliwatatanisha watahiriwa kupata ujumbe uliokusudiwa katika nyimbo za jando za Watachoni. Ilikuwa dhahiri kuwa jamii hii ya Watachoni hutumia mtindo wa majigambo uliowafurahisha watahiriwa japo hawakuelewa ujumbe kusudifu ilivyobainishwa kwa nadharia ya baada ya umuundo. Kwa jumla, majigambo yanayojitokeza katika nyimbo za jando hueleweka katika miktadha ya matumizi yake na huwawezesha watahiriwa kuwa na umilisi wake kuthibiti umuhimu wake hivyo uwapa ujasiri wa kuilinda na kuendeleza kutoka vizazi hadi vizazi mbeleni.

Taswira

Taswira huwa mtindo wa uwasilishaji katika mawasiliano ambao humfanya msomaji au msikilizaji kuzua picha akilini mwake kutokana na utanzu husika wa kisanaa. Utafiti huu umebainisha kuwa matini zinazootokana na nyimbo za jando kupitia Tanzu zake za nyiso na maghani huwapa picha zinazotoa mafunzo ya jando. Kutokana na

msailiwa BBU 1, jando hulenga kuwapa watahiriwa ujasiri kutokana na picha za matokeo ya kustahimili au kuogopa jando katika jamii ya Watachoni. Vilevile, zinawawezesha kuwa na picha ya asili ya jamii na mila yao, misafara na shughuli mbalimbali za Watachoni hasa wakati wa kutekeleza mila na malengo ya jando kuhusiana na majukumu wanayoandaliwa watahiriwa kwayo katika utu uzima wao. Mtindo huu wa taswira hukamilika katika mawasiliano haya ya nyimbo za jando kulingana na namna wasanii wanavyotumia lugha kuwasilisha huu ujumbe wao. Kulingana na Senkoro (1988), lugha inayosemekana kuwa ya kishairi na au nyimbo aghalabu huwa ya kitaswira. Mtindo huu hutumika kuzifanya nyimbo ziwe hai na zenye uhalisia zaidi. Waimbaji hutumia mtindo huu kuzinasa hisia za hadhira kwa kuwapangia maneno yanayoumba picha kamili katika akili zao kuhusu miktadha ya matumizi ya nyimbo za jando zinazorejelewa. Lugha hii huwapa wasikilizaji picha kamili za inavyosimulia na kufafanuliwa fanani. Mtindo huu wa uwasilishaji umejidhihirisha katika mawasiliano haya ya nyimbo za jando katika jamii ya Watachoni kutokana na uchanganuzi wake katika utafiti huu.

Katika mawasiliano ya wimbo MNNJ 4, taswira imejengeka akilini mwa mtahiriwa kutokana na mada ya ushauri huu *ungeuliza*. Kulingana na msailiwa MU 1, inabainika kuwa mtahiriwa hufaa kupata ushauri kuhusu tohara ya jando kutoka kwa watu mbalimbali kabla ya kufanya uamuzi kushiriki. Taswira inayojitokeza hapa kulingana na msailiwa wetu ni kuwa kabla ya wazazi Hata hivyo, uelewa huu huwa na utelezi mwingi kutokana na taswira inayotokana na tafsiri ya maana ya kibinafsi dhidi ya maana inayokusudiwa na waimbaji walio wataalamu wa jando. Kuna uwezekano kuwa hawa wataalamu hawakuwa makini watahiriwa wapate maana ya mafunzo haya kwa kuwa jamii ya Watachoni ni jamii siri.

kulikubali ombi la mtoto wao kutahiri kutokana na azimio lake, yafaa waweze kumuuliza ili wapate uhakika iwapo ameamua kweli inavyojitokeza katika mishororo ya 5 na 6. Mawasiliano katika wimbo huu hudhihirisha kuwa mtahiriwa akishapewa rufusa na wazazi wake hawezi kurudi nyuma tena; lazima alibeba jukumu hili muhimu katika mila na kuhakikisha kuwa anaitimiza kwa ushupavu. Aidha msailiwa MU 1 alisema kuwa suala la kutahiri huwa muhimu na huwa lazima mtahiriwa atafute ushauri wa watu muhimu katika jamii wanaomwezesha kufanya matayarisho na hatimaye kuikamilisha inavyojitokeza katika wimbo MNNJ 4 hapa;

Kitachoni

Fanani: Eehee haahaa x2

Hadhira: Eehee, haahaa, haaa siwali wareva, haahaa, haaa ungeuliza,

Fanani: Musinde siwali wareva mayi x2
ungeuliza mama x2

Hadhira: Eehee, haahaa, haaa siwali wareva, haahaa, haaa ungeuliza,

Fanani: Musinde siwali wareva Omutoto, ungeuliza mila x2

Hadhira: Eehee, haahaa, haaa siwali wareva, haahaa, haaa ungeuliza,

Fanani: Papa siwali wareva omwana x2
ungeuliza mtoto x2

Fanani: Senje siwali wareva omwana x2
ungeuliza mtoto x2

Kiswahili

Eehee haahaa x2

Eehee,

Zunga

Eehee,

Zunga

Eehee,

Baba

Shangazi

Mtindo wa Utohozi

Data za utafiti huu zinabainisha matumizi ya aina zote za utohozi kutokana na nyimbo za jando inayorejelewa pamoja na maelezo tunayoyapata kutoka kwa wasailiwa wetu. Kwa mujibu wa Musota (2016), kuna viwango vitatu vya utohozi mathalani wa moja kwa moja, wa tafsiri na wa kubadilisha maneno yaliyokopwa kwa kuzingatia viwango vya lugha pokezi. Utafiti umebainisha kuwa

lugha ambayo imetumika katika mawasiliano ya nyimbo za jando yametoholewa kutokana na mtagusano unaobainika kuwepo kati ya jamii ya Watachoni na jamii zingine walizokumbana nazo nyakati za uhamaji na shughuli zingine kama vita, ndoa, ufumaji wa vifaa vya kitamaduni kati ya mengine. Mtindo huu huwa utaratibu wa kuunda istilahi kwa kuyabadili maumbo ya maneno yaliyokopwa kutoka lugha chanzi ili yalingane na kuoana na fonolojia ya lugha lengwa. Ni dhahiri kuwa neno linalotoholewa hutamkwa kwa utaratibu wa lugha pokezi, hata hivyo maana ya neno lililotoholewa hubakia ileile ya awali (Matinde 2012). Maelezo haya yamethibitishwa kwa matini ya nyimbo za MNMJ 6, MNMJ 7 na MNMJ 9 kama zinavyotumika katika utafiti huu.

Katika wimbo MNMJ 9, maneno mengi yanayotumika yametoholewa kama ilivyo katika kifungu kifuatacho:

Kitachoni

Fanani: Khwecha Echeng'alali,
Hadhira: Haahaa,
Fanani: Khwatukha Esengeli,
Hadhira: Haahaa Cheputalang'...Haahaa Cheputalang'
Fanani: Khwambukha Obulalo,
Hadhira: Haahaa Cheputalang'... Haahaa Cheputalang'

Kiswahili

Tukaja Echeng'alali
Haahaa
Tukafika Esengeli
Tukavuka daraja

Kwa mujibu wa maelezo ya msailiwa MU 8, neno *esengeli* limetoholewa kutoka lugha ya Kalenjin Senger linalobeba maana anuai. Amesema kuwa neno hili limetoholewa kurejelea malighafi yaliyotumiwa na Watachoni wakati huo kutengeneza vifaa muhimu vya kutekelezea shughuli mbalimbali za jando kama vile kengele za watahiriwa, visu vya kutahiri, mikuki kati ya vingine vingi. Hivi vifaa vinatumika kwa kazi hii ya kutahiri hadi sasa katika jamii ya Watachoni. Haya yalifanyika Watachoni walipokuwa wameweka katika makazi ya Mbayi, Sirikwa huko Uasin Gishu kabla ya kuvuka Mto Nzoia na kuingia Mlima Elgon. Vilevile, jina hili linatokana na jamii ya Sengeli au Sengwer

iliyoishi mahali palipoitwa Sengeli. Ochieng' (1995b) anathibitisha kuwa Sengwer huwa jamii ya Wakalenjin inayoongozwa na kiongozi wao, Sengeli. Kwa vile walikuwa wanaishi pamoja na Watachoni, Sebei, Pokot, Tugen, Kony wakati huo, Watachoni walilitohoa neno hili na kuanza kulitumia hadi wa leo. Kulingana na Wandiba (1995), Sengeli ni kundi la watu wa jamii ya Kalenjin hivyo hali inayobainisha esengeli ni neno linalotokana na jamii hii kubainisha kuwa wamechangamanikana na Watachoni wakati fulani hapo awali. Nguzo za nadharia ya baada ya umuundo ya maana binafsi, iliyokusudiwa na ya maana kamili ya matini ilielekeza uelewekaji wa maneno na istilahi hizi toholevu katika nyimbo za jando.

Katika wimbo MNMJ 7, neno *Aechelayo* linalosemekana kuwa linatokana na neno la Kisabaoti *aejelayo* linalomaanisha *tunaenda kumtahiri masewa* ili awe kama simba. Neno *Layo* linalomaanisha simba katika lugha ya Kisabaoti ilhali Watachoni humuita simba *inyatuni* huku Wabukusu wakimuita *etalang'* hivyo kuthibitisha kuwa kweli Watachoni walitohoa kutoka lugha ya Kikalenjin pakubwa. Kwa jumla, mtindo wa utohozi ulibainika kutumika katika nyimbo hizi za jando ili kukidhi mahitaji ya msamiati mwafaka wa kufaulisha mawasiliano katika shughuli za jando kupitia nyimbo za jando kwenye jamii ya Watachoni. Jambo lisiloeleweka kwenye muktadha huu ni kwa nini Watachoni waliamua kutohoa istilahi zilizokuwa na visawe katika lugha yao ambayo vilivyoeleweka bayana na watahiriwa na jamii.

Tashihisi

Huu mtindo wa tashihisi ulibainika kutumika pakubwa katika nyimbo za jando katika jamii ya Watachoni ili kuyapa maana na kuziwezesha nyimbo hizo kufikia makusudio yake. Katika mtindo huu, utafiti huu ulibainisha kuwa na hali ya ulinganisho lakini hapa vitu visivyo na uhai au vyenye sifa za kibinadamu hupewa sifa, tabia, sura au matendo ya kibinadamu. Pia katika mtindo

huu viitu visivyo hai huonekana kusema na kutenda kama viumbe hai. Katika wimbo wa nasaha MNMJ 1, msailiwa MJM 1 alibainisha kuwa aghalabu mjomba humtaka mtahiriwa asimame bila woga ngariba anapomtahiri kwa kumwambia hivi:

*Miaka mikaka na mikaka, hatuogopi kisu cha ngariba,
Ukiogopa, uoga huo ni wa kwenu, kamwe sisi hatuogopi,
Ukishafika madhabahu ya kutahiri, usimame tisiti, kisu
kikutembelee,
Uwe jasiri, kisu kitembee bila kushituka,
Mimi mjombako, sikuogopa kamwe.*

Kawaida, kisu hakina uwezo wa kutembea kivyake juu ya kitu kama anavyofanya kiumbe mwenye uhai kama kibinadamu. Mtahiriwa anapokuwa anatahiriwa kwa kukatwa ngovi ya mboo yake, anastahili kumruhusu ngariba afanye kazi yake amalize bila kuonyesha woga wowote. Kujitikiza au kujiguna kwa mtahiriwa huashiria woga na ndiyo maana watahiriwa hupewa fimbo baada ya kuandaliwa mtoni ili aishike kwa mikono miwili ikiwa mabegani. Msailiwa MJM 1 matini katika mshororo wa 3 na 4 humhimiza mtahiriwa kuwa jasiri anapopitia tohara hii. Aidha anahimizwa awe jasiri anakapokabiliwa na majukumu na changamoto katika maisha yake ya baada ya jando (ukubwani). Kwa hivyo kisu kimehaishwa katika wimbo huu ili kuwasilisha maana kuu ya ujasiri katika mawasiliano haya ya nyimbo za jando ya Watachoni. Inakamilishana na mawaidha yanayomtaka mtahiriwa aweze kuwa jasiri katika nyimbo zingine ambazo zimetumika katika utafiti huu hasa katika nyimbo za MNNJ 6, MNMJ 1, MNMJ 2 na MNMJ 3. Katika jamii ya Watachoni, mtu anayeogopa au anayekosa kutahiri huchukuliwa kuwa mtoto mdogo hata akiwa na umri wa mtu mzima. Mtazamo huu hufanya usemi unaohaisha kisu kuwa muhimu kwa watahiriwa wanaofanya bidii kuafiki maelekezo ya nadharia ya ubabe dume kwa nguzo za ujasiri, uthabiti, umilisi na kujiamini ambazo ndizo hupima ukamilifu wa mwanamume aliyepitia jando.

Kutokana na uchanganuzi wa mtindo huu, inabainika kuwa mawasiliano ya nyimbo za jando huwawezesha watahiriwa kupata ujasiri wa kupashwa jando. Tumemuona mjomba akimtaka mtahiriwa aache kisu cha ngariba kimtembelee, ilimbidi mtahiriwa kujiamini, kuwa thabiti na kuonyesha heshima na maadili bora kwa jamii yake. Kutokana na kitendo hiki, ni dhahiri kuwa watahiriwa huyaelewa mawasiliano na mafunzo yanayotokana na mtindo huu katika nyimbo za jando. Hata hivyo, baadhi ya tashihisi hazieleweka kabisa japo zinabeba mafunzo makuu katika mawasiliano haya ya jando haieleweki kwa nini lugha hii imeendelea kutumika kwa muda mrefu. Suala la umuhimu wa ushirikiano unaoleta ufanisi katika maisha umeangaziwa na kusisitizwa japo lilivyoangaziwa halikuwa bayana kwa watahiriwa. Kwa mfano, mawe matatu yanayopanda kijiti, kisu na emotia kutembelea pamoja na pembe za ng'ombe kutembelea pamoja haikuwa na maana bayana kwao. Ufafanuzi na maelekezo ambayo hayakutolewa na viongozi wa mawasiliano haya. Kwa jumla, mtindo huu unahitajika kuchangia ufanisi wa mafunzo ya jando lakini ulikuwa na upungufu unaohitajika kuushughulikia ili kuboresha mawasiliano haya ya jando.

Uradidi

Deta ya utafiti huu ilibainisha matumizi ya uradidi kama mtindo katika nyimbo za jando zilizorejelewa kwa wingi. Uradidi ukiwa kanuni au utaratibu wa kuunda neno au maneno mapya kwa namna ya kurudia sehemu ya neno au neno zima katika lugha umebainika kusheheni takribani nyiso na maghani yote yanayorejelewa katika utafiti huu. Kwa mujibu wa msailiwa MU 1, ujumbe katika nyimbo za jando huwa dhahiri tu iwapo umerudiwarudiwa hasa katika mikarara yake kwa madhumuni ya kutilia mkazo au kusisitiza ujumbe wake. Kwenye nyimbo husika. Vilevile uradidi huu umebainika kutumika sana ili kuleta mdundo, kiimbo na mahadhi

katika nyimbo na maghani ya jando inavyobainisha katika uchanganuzi wa sehemu hii. Kulingana na Rubanza (1996), uradidi ambao huwa njia ya kuunda maneno mapya katika lugha kwa kurudufu au kwa maneno mengine. Kwake Massamba (2009), uradidi ni urudufu kamili au urudufu nusu wakati neno lote au nusu linaporudiwa mtawaliwa. Matinde (2002) amedokeza kuwa utaratibu unaotumika katika kuunda maneno ambayo sehemu yake au neno lote hurudiwa na kuunda neno au msisitizo fulani huwa ni uradidi. Aidha, mwingiliano uradidi hubainika pale ambapo neno la mwisho la fanani linarudiwa na hadhira huku baadhi ya maneno hayo yakiwasilisha tanzu tofauti na utanzu husika. Mutembei (2015) anakataa kuwa siyo kurudiwarudiwa maneno, vifungu na matendo ndiyo inayoleta uradidi bali ni muhtasari wa maana unaobebwa na sehemu husika inayorudiwarudiwa yaani ujumbe kusudufu. Maelekezi haya yatatuongoza kuainisha namna mtindo huu umetumika katika nyimbo za jando na kuchangia kuafiki malengo ya tohara hii kwa watahiriwa wake. Uradidi ndio unaoleta haja ya matumizi ya nadharia ya ubabe dume na baada ya umuundo ili kuweka bayana maana ya matini yanayojitokeza katika nyimbo za jando zinazotumika katika jamii ya Watachoni.

Takribani nyimbo zote katika mawasiliano haya ya jando zinadhahirisha matumizi ya mtindo huu wa uradidi. Kulingana na msailiwa MKJ 1, inathibitika kuwa mawasiliano ya nyimbo za jando huwa na viongozi wanaowashirikisha wanajamii katika kuyaendeleza mawasiliano haya. Ushirikisho wa hadhira hutilia msisitizo ujumbe husika na kufanya uwe wa kuburudisha kwa watahiriwa na kwa jamii ya Watachoni yote kwa njia ya kurudiarudia maneno na usemi unaobeba ujumbe muhimu. Kutokana na utafiti huu, inabainika kuwa kila wimbo huwa na maneno, vifungu vya maneno ambavyo hurudiwarudiwa kwa ajili ya kuusisitiza ujumbe au kuleta mdundo wa kuburudisha ifuatavyo;

- MNNJ 1 Haahaa
- MNNJ 2 Hohowe
- MNNJ 3 Hahaa, hohee
- MNNJ 4 Haahaa
- MNNJ 5 Heehee na haahaa katika kiitikio
- MNNJ 6 Hehehee, heehee, hehe
- MNNJ 7 Haahaa, haahaaa
- MNNJ 8 Haahaa, haaaa
- MNNJ 9 Haahaa, haaahaa, haaaaa
- MNNJ 10 Viitikio tofautofauti

Uradidi katika mikarara na viitikio vya nyimbo za jando zilibainika kudhahirisha namna washiriki wanavyofurahia uimbaji na ughanaji wa hizo nyimbo. Kwa hivyo mtindo huu husheheni umuhimu mkubwa unapotumika katika nyimbo hizi na uelewekaji wake hasa katika kukamilika kwa shughuli za jando kulingana na miktadha ya matumizi yake inavyodhahirika katika sehemu mbalimbali za utafiti huu.

Kutokana na ubainishaji na uchanganuzi wa mtindo huu, ilibainika kuwa umetumika kuwasilisha ujumbe katika mawasiliano ya nyimbo za jando. Matumizi ya takiriri hulenga kutilia mkazo ujumbe unaolengwa katika mawasiliano haya. Takiriri hii hasa huwa bayana katika maombezi ya jamii wanapokuwa wanawatoa watahiriwa jandoni. Vilevile, takiriri inabainika kutumika kama viitikio katika takribani nyimbo na maghani yote katika utafiti huu hivyo huwawezesha watahiriwa na jamii kutilia maanani ujumbe wake. Mtindo huu pia umebainika kuleta mahadhi na mdundo katika mawasiliano haya na kuburudisha hadhira yake hivyo kunata nathari zao. Hata hivyo, matumizi ya baadhi ya vifungu vya maneno ya takiriri yalihatiji maelezo na ufafanuzi ili watahiriwa waelewe maana kusudifu. Wasemavyo Njogu na Chimerah (1999), utanzu wa sanaa kama ushairi au wimbo haufai kutumia msamiati unaozidi uwezo wa walengwa hasa tunapowalenga watahiriwa ambao wengi huwa na umri na uelewa mdogo. Kwa misingi ya nadharia tumizi katika huu utafiti, mtindo huu umebainika kutumika

kubainisha namna ya kuwachochea watahiriwa kumudu jando na kutekeleza majukumu yao ya utu uzima kwa umahiri, ujasiri huku wakiwa wameelewa maana ya matini inavyoelekezwa kwa nguzo za nadharia ya baada ya umuundo pamoja na nadharia ya ubabe dume.

Jazanda

Huu ni mtindo ambao vitu viwili hulinganishwa moja kwa moja bila kutumia viunganishi vyovyote. Mtindo huu ulibainika kutumika katika nyimbo za jando ili kufaulisha malengo yake maalum. Kwa mfano, katika wimbo MNNJ 4, jazanda imedhihirika kutumika kupitia neno *omutoto*. Kulingana na mtafiti BBU 1, *omutoto* huwa aina ya mti unaoitwa mkuyu kwa Kiswahili na huwakilisha mila ya Watachoni. Aliongeza kuwa neno hili lilitumika katika wimbo huu kuwakilisha mila ya Mtachoni. Mti na mila huwa maneno yenye uhusiano wa kimaana usiojitokeza moja kwa moja isipokuwa kijazanda. Katika mshororo wa kwanza, mtahiriwa anaambiwa kuwa *zunga ungemwuliza omutoto* kuthibitisha umuhimu wake katika jamii ya Watachoni sawa na jamii nyingi za Kiafrika. Maana ya jazanda hii imebainika kuwa telezi kwa watahiriwa wengi kutokana na msailiwa huyu BBU 1 hivyo basi nguzo za nadharia ya baada ya umuundo ya maana binafsi, iliyokusudiwa na maana kamili ya matini ni muhimu kutumiwa kuelewa maana ya ujumbe wa wimbo huu.

Kwenye wimbo MNNJ 8, neno *omunyolo* limetumika kijazanda. Kulingana na mtafitiwa MMT 3, yeyote anayeogopa jando, hufaa kuhamia kule ambako hawafanyi tohara ya jando. Kwa Mtachoni yeyote aliyekataa au kuogopa kutahiri aliambiwa hivyo ili kumkumbusha kuwa jamii ya Watachoni hawaogopi jando kama ilivyo katika MNMJ 1, 2, 3. Wimbo huu unabainika kuimbiwa mtahiriwa ambaye baada ya kuimudu jando kwa ujasiri hivyo huwa ni wa kusherehekea ushindi wake pamoja na wazazi wake. Vilevile, huendelea kuwakumbusha Watachoni kuwa mila

yao hutarajia wanaume kutahiri kwa ujasiri ndiposa walioogopa huambiwa kuwa wahamie kule ambako hakuna mila ya kutahiri kama ilivyokuwa kwenye jamii ya Wajaluo hapo awali inavyojitokeza katika wimbo huu wa MNNJ 8 ifuatavyo:

Kitachoni

Fanani: Khwakhaseva omunyolo haaaa, Tumemtahiri Omunyolo haaaa

Hadhira: Haahaa lelo, ha!

Fanani: Mayi wo omwana haaaa,

Hadhira: Haahaa lelo, ha!

Fanani: Mayi hali hena haaaa,

Hadhira: Haahaa lelo, ha!

Kiswahili

Haahaa lelo haaaa

Mama wa Mtoto haaaa

Haahaa lelo, ha!

Mama yuko wapi haaaa

Haahaa lelo, ha!

Ni dhahiri kutokana neno *omunyolo* limetumika kijazanda katika wimbo huu wa jando namna ulivyonukuliwa. Kwa maana ya kawaida, umunyolo hurejelea sehemu ya mboo inayokatwa mvulana au mwanamume anapotahiri. Mtu anaporejelewa kama *omunyolo* katika lugha ya Kitachoni humaanisha Mjaluo na yule Mtachoni anayeogopa kutahiri hukejeliwa na kuimbiwa aende *ebunyolo* yaani Ujaluoni. Kwa hivyo mtahiriwa anapofaulu kukabiliana na kisu cha ngariba, jamii husherehekea kwa mwanzo kutoa sehemu ya mboo (ngovi) kwa maana ya kawaida lakini pia hushangilia mtahiriwa kwa kuwa amefanywa mwanamume na kukoma kuwa *omunyolo* (jazanda). Kwa hivyo mtindo huu uliwawezesha viongozi wa jando kuwachochea watahiriwa wanapowaandaa kwa majukumu ya kuilinda na kuiendeleza mila ya jamii.

Kwa jumla, mtindo huu wa jazanda umefaulu kuwasilisha ujumbe kwa watahiriwa katika mawasiliano ya nyimbo za jando katika jamii ya Watachoni. Kwanza, watahiriwa wanafurahia mawasiliano haya kutokana na picha ya vitu, hali, matukio yanayohusishwa na mafunzo yanayotumiwa katika nyiso na maghani haya. Vitu kama pembe kubwa, mawe matatu, mti wa mkuyu (*omutoto*), ndege mbalimbali kama (*shore, tai, kipanga, mwewe*), wanyama (*chui, fuko, mbwa, kiharahara*), matukio kama vile

kutazama mashariki kati ya mengine viliwachangamsha. Hizi picha ziliwavutia watahiriwa na kubainisha maana kutokana na uzoovu wa watahiriwa kwa kuwa walikuwa wamewaona, kusoma au kusikia kuwahusu. Hata hivyo, ilikuwa dhahiri kuwa matumizi yake ya kijazanda ilibainika kutatiza uelewa wa watahiriwa hali ambayo ilionekana kuwanyima watahiriwa nafasi ya kufaidika kwa mafunzo muhimu yanayotokana na nyimbo hizi za jando ili wayatumie kumudu jando inavyostahili na katika kutekeleza majukumu yao ya kijamii katika utu uzima wao baada ya jando.

Mtindo wa Mwingiliano matini

Data ya utafiti huu ilidhihirisha matumizi ya mtindo wa mwingiliano matini katika nyimbo za jando za jamii ya Watachoni. Mwingiliano matini kama mtindo huonyesha kutumika kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilisha utanzu mwingine kwa mfano wimbo au kipande cha wimbo kinapotumika ndani ya hadithi (Senkoro 2011). Vilevile, mwingiliano matini hurejelea ule uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi kama vile matumizi ya ngoma, barua, masimulizi, majibizano na vichekesho. Kulingana na msailiwa MU 1, nyimbo za jando ya Watachoni ni sanaa ambayo kutumia mtindo huu wa mwingiliano matini kutoka katika maeneo mengine kama vile visasili, hadithi na vitabu vitakatifu ambavyo vinaelekeza ukuzaji wa maadili katika jamii.

Data ya utafiti huu inadhahirisha matumizi ya mtindo wa mwingiliano matini inayojitokeza katika nyimbo (nyiso na maghani) ambazo zimerejelewa humu utafitini. Katika wimbo wa MNNJ 9 ilibainisha namna Watachoni walivyovuka Mto Jordan walipokuwa wakihama kutoka Misri na kuelekea katika makao yao ya sasa. Kwa mujibu wa kisaili hiki, mtafitiwa MKJ 1 amedokeza kuwa Watachoni walikuwa pamoja na Musa wa Biblia walipovuka Mto Jordan. Anaongeza kudai kuwa mila ya

jando ya Watachoni huendelezwa kulingana na kanuni zinazotokana na mawe matatu yaliyookotwa kwenye mto Jordan inavyojitokeza katika kifungu cha wimbo huu MNNJ 9;

Kitachoni

Fanani: Musa walakaya,

Hadhira: Haahaa Cheptalang'

Fanani: Amachi kasingila

Hadhira: Haahaa,

Fanani: Khwatola amachina

Hadhira: Haahaa Cheptalang'

Fanani: Amachina kataru

Hadhira: Haahaa,

Fanani: Karakanga olusala

Kiswahili

Musa akasema

Haahaa Cheputalang'

Maji yakasimama,

Haahaa,

Tuliokota mawe,

Haahaa Cheputalang'

Mawe matatu,

Haahaa,

Yanayopanda kijiti,

Kutokana na nukuu hii, mtafitiwa MKJ 1 (ametajwa) alibainisha kuwa mawe yale matatu ndiyo yanayotumika kupanda omutoto (mkuyu) unaosimamia mila ya Watachoni. Maelezo haya huingiliana na matini kwenye Biblia, kitabu cha Kutoka mlango wa 14 kinazungumzia habari za Musa alipowaongoza wana wa Israeli kuvuka mto wa Yordani wakiutoroka utumwa wa Faraho. Msailiwa MKJ 1 anabainisha kuwa kisaili cha Watachoni kinadhahirisha kuwa Watachoni walihama kutoka Misri hivyo walikuwa pamoja na Wana wa Israeli waliuvuka Mto wa Yordan wakiongozwa na Musa Mungu aliposimamisha maji ili wapite salama. Wana wa Israeli wakiwemo Watachoni waliulizwa kuokota vitu walipovuka ili iwe ukumbusho kwa miujiza waliokuwa wamefanyiwa na Mungu. Utafiti huu ulionyesha kuwa Watachoni waliokota mawe matatu wanayoyatumia kutengenezea na kuendeleza mila yao ya kupanda *kijiti*. Kutokana na msailiwa BBU 1, mila ya Watachoni ilisemekana kuwa ilitokana na Mungu mwenyewe kupitia kwa Musa, hivyo ni takatifu namna inavyoshikiliwa na jamii hiyo. Msailiwa huyu alidai kuwa mila ya jando huongozwa kwa kanuni bainifu ambazo huhifadhiwa kwenye kitabu cha kanuni za Watachoni zinazosomewa

watahiriwa wakibarikiwa wakati wa kuwatoa jandoni kwenye *esitabicha*. Nadharia ya baada ya umuundo ilidhihirika kuwa muhimu katika kuelewa matini katika wimbo huu. Nguzo ya maana binafsi iliwapa watahiriwa kupata maana yao binafsi huku maana iliyokusudiwa na maana kamili ya matini ikiwakwepa wakati huu wa jando lakini ikaeleweka katika maisha yao ya baadaye wanaposhiriki katika utekelezaji wa majukumu yao baadaye.

Kutokana na utafiti huu, ni dhahiri kuwa huu mtindo wa mwingiliano matini umetumika na kachangia pakubwa kuyaendeleza na kuyachanganua mawasiliano haya ya nyimbo za jando ya Watachoni. Umefaulu kuonyesha uhusiano wa karibu uliopo kati ya matini yanayoainishwa kwenye nyimbo za jando na matini katika maandiko ya neno la Mungu hasa kwenye Biblia. Hata hivyo, matumizi ya mtindo huu katika mawasiliano haya yanakanganya uelewa kamili wa watahiriwa licha ya wao kuwa ndio wanaolengwa kwayo. Wengi wao kwa misingi ya wanayojifunza kanisani na misikitini wanaelewa kuwa mila ya jando huwa ni kinyume na mafunzo ya kidini kwa kuwa hurejelewa mara nyingi kama dhambi katika mafunzo ya Kikristo. Kutokana na mtindo huu wa mwingiliano matini, imethibitika kuwa mafunzo na matendo mengi yanayotekelezwa huwa na uhusiano wa karibu kwani zote hulenga kuwatayarisha wahusika wao kwa majukumu ya baadaye maishani mwao kupitia mafunzo maalumu na kutoa baraka kwa walengwa. Nadharia ya baada ya umuundo ilielekeza watahiriwa katika kubainisha maana ya matini katika nyimbo za jando kwa kurejelea nguzo za maana ilnayokusudiwa na maana kamili ya matini.ya matini.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Utafiti huu uligundua kuwa mitindo na lugha inayotumika katika uwasilishaji wa nyimbo za jando ndiyo inayoyafanya kukidhi mahitaji ya tohara hii pamoja na

kuipa upekee wake. Vilevile, ilibainika kuwa uwasilishaji huu hufanywa na watu mahsusi walio na uwezo wa kipekee wa kupitisha ujumbe wa kijamii kulingana na matarajio ya mila ya Watachoni. Anavyosema Lihraw (2010), wawasilishaji wa nyimbo za jando walikuwa na uwezo usio wa kawaida kutokana na kupagawa na roho ya mila inayowapa nguvu za kiungu kuwasilisha mafunzo muhimu ya jando. Nguvu hizo huwafanya watumie maneno yasiyoeleweka moja kwa moja bali katika miktadha yake maalum. Kulingana na Wanjala (2011), njia ya kuwasilisha utanzu wa fasihi simulizi kama ushairi hutegemea upokeaji na utenda kazi wake hutegemea mitindo inayotumiwa kuuwasilisha. Naye Mohamed (2011) anasema kuwa mitindo ya uwasilishaji hulenga ujumbe unaopitishwa kuafiki malengo yake ipasavyo kwa kutegemea mawazo na mielekeo ya walengwa. Mitindo iliyotumika katika mawasiliano haya ya nyimbo za jando ilikuwa: nyimbo, maghani, majigambo, uradidi, muingilianomatini, maigizo, utohozi na taswira. Vilevile, mitindo ya jazanda na tashihisi pia ilitumika.

Mapendekezo: Ilibainika kuwa asilimia kubwa ya mahafala wa jando wanapata changamoto kuyaelewa mafunzo katika nyimbo za jando na kuyatumia baadaye kutekeleza majukumu yao ya utu uzima. Utafiti huu unapendekeza kuandaliwe warsha kwa mahafala wa jando kila baada ya miaka minne ili kuwahamasisha kuhusu kanuni, mitindo na dhima za nyimbo katika shughuli za jando ya jamii ya Watachoni. Viongozi wa shughuli za jando wanafaa wapitishiwe katika semina za mara kwa mara kuangazia na kuimarisha utendaji wao katika uteuzi wa matini, mitindo na lugha mwafaka za utoaji mafunzo kupitia nyimbo za jando katika jamii ya Watachoni. Aidha, viongozi wajiadili na kuwekea wahudumu wa jando viwango fulani vya kitaaluma katika masuala ya jando ili kuhakikisha kuwa watahiriwa wanapata mafunzo yanayoambatana na kanuni za mila ya Watachoni.

MAREJELEO

- Alembi, E. B. (1999). *Understanding Poetry*. Accacia Publishers Limited.
- Barasa, K. & Sure, K. (1993) (*add initials*). *Gateway Secondary Revision, ENGLISH*. Longman Kenya Ltd.
- Derrida, J. (1966). “Structure, Sign, and Play in the Discourse of Human Science” and Presented in the Languages of Criticism and Science of Man in 1967.
- Gill, J. & Waters, M. (2009). Poetry and Autobiography, *Life Writing* 6(1): 1-9
- Gikandi, S. (2003). *Encyclopedia of African Literature*. Routledge.
- Jilala, S. (2012). *Sitiari za Ukimwi na Mapenzi katika Mashairi ya Bongo Fleva*.
- Kahigi, K. K (1975). *Ushairi: Mtazamo wa Kisayansi katika Kiswahili: Juzuu 45/1*. TUKI, Chuo Cha Dar-es-Salaam.
- Kakai, P. W. (1992). *Social Concepts in the Initiation Rituals of the Abatachoni: Historical Study*. M. A Thesis, Kenyatta University, Kenya.
- Lihraw, D. O. (2010). *The Tachon Peoples: History, Culture and Economy*. Entrepreneurship Development Institute (EDS).
- Macha, N. E. (2013). *Mwingiliano Matini katika Tendi*. chomboz.blogspot.com
- Maclennes, J. (1998). *The End of Masculinity*. Buchingham Open University Press.
- Madumulla, J. S. (1989). “Another Look at Kiswahili Scholarship” *Kiswahili* 56, 10 – 24.
- Masanjila, Y. P., Kihore, Y. M., & Massamba, D. P. B. (2009). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam. TUKI.
- Massamba, D. P.B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar-Es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Natharia. Kwa Sekondari, Vyuo Vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- Mattteru, J. (1981). *Fasihi Simulizi na Uandishi makala ya semina ya waandishi wa Kiswahili Dar-es-Salaam*.
- Mayoka, J. M. (1986). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Tanzania Publishing House.
- Mazrui, A., & Syambo, B. K. (1992): *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi. East African Educational Publishers.
- Mburu, J.M (2014). *Fani Katika Nyimbo Teule za Anastacia Mukabwa. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi*. Miricho, M., Nganje, D., Kobia, J., & Wacira, D. (2008). *Distinction Kiswahili for Primary Teacher Education*. Kenya Literature Bureau.
- Mohamed, S. A. (2011). *Janga La Werevu*. Longhorn Publishers.
- Momanyi, C. (2007). “Patriarchal Symbolic Order. The Syllables of Power Accentiated in Waswahili Poetry.” *The Journal of Pan African Studies*, 1,8
- M’Ngaruthi, T. N. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni: Kitabu cha Walimu na Wanafunzi* (Shule na Vyuo). The Jomo Kenyatta Foundation,

- Mulokozi, M. M. (1982). 'Nafasi ya Nyimbo za Fasihi Simulizi katika Jamhuri Inayobadilika':
Musira, W. (2015). "Utanzu wa Fasihi Simulizi" Makala katika Swahilithub.com (2015).
- Musota, K.E. (2016). Utohozi wa Msamiati Kutoka Kiswahili Hadi Ekegusii. Tasnifu ya
Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Mutembei, A. K. (2012). *Korasi Katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uihakiki*. TUKI.
- Mwaniki, K. W. (1986). *Categories and Subsistence of Embu Traditional Songs and Dances*. Kenya
Literature Bureau
- Nikola (1966). *A History of Abaluyia*. Nairobi. UON.
- Njogu, K., & Chimerah, R (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.
- Ochieng, W. R. (1975). *An Outline History of the Rift Valley of Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Okumba, M. (2001). *Oral Literature of the Luo*. East African Educational Publishers. Osogo, John Nikola
(1966). *A History of Abaluyia*. Nairobi. UON.
- Rubanza, Y. I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania
- Senkoro, F. E. M. (1981). *Fasihi na Jamii*. Dar-es Salaam, Press and Publicity Centre.
2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.
(1988). *Ushairi: Nadharia na Uihakiki*. Dar-es-Salaam University Press.
- Wamitila, A.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books. (2006).
Kamusi ya Ushairi. Vide - Muwa Publishers Ltd.
(2008). *Kanzi ya fasihi 1. Msingi na Uchanganuzi wa Fasihi*. Dar-es salaam University Press.
(2010). *Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi : Vide Muwa
(2013). *Tiki maji*. Vide-Muwa Publishers Ltd.
- Wandiba, S. (1985). *History and Culture in Kenya*. Nairobi: Gideon S. Were Press.
- Wanjala, F. S. (2015). *Mwingilianotanzu Katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano Embalu na Mwaka wa
Kogwa*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- White, J. (1984). *When Words Lose Their Meaning: Constitution and Reconstruction of Language
Character and Community*. The University of Chicago Press.